




Mwizi wa Ndizi

kujumlisha na kutoa
namba hasi

Age
Umri
7+





Baada ya kucheza na marafiki zake Kiduchu alikuwa amechoka sana na alihisi njaa!

Koba alimpa Kiduchu ndizi tatu maana yeye alikuwa amefunga. Kiduchu alimshukuru Koba na kumuahidi kuwa atamrudishia jioni.



“Sasa nimeshiba,
bora niende nikatafute ndizi
za kumrudishia Koba.”





Akaenda gengeni na
kumuomba Mzee Kigo
amkopeshe ndizi tatu.




Akamwambia atakuja
baadae na ndizi nne, ndizi
tatu za kulipa deni na
ndizi moja ya ziada, kama
zawadi kwa Mzee Kigo.



Mzee Kigo alitaka
kujua kwa nini Kiduchu
alihitaji ndizi nyingi hivyo.





“Koba alinipa ndizi tatu na nimekula zote. Nilimuahidi nitamrudishia.

Kwa hiyo ananidai ndizi tatu. Hiyo inamaanisha nina ndizi **hasi tatu.**”

-3



Mzee Kigo akampa Kiduchu
ndizi tatu nzuri zilizoiva.



Alikimbia kumtafuta Koba,
lakini alijikwaa kwenye gogo.





Ndizi zake zikaruka juu na kupotea!



Otea mnyama gani mdogo mdogo
na mjanja mjanja alizidaka?




Muda mfupi tu Kiduchu alikutana
na Ngedere akiuza ndizi.



Ngedere akamwambia kuwa atampa ndizi wabadilishane na pilau. Ngedere akamwuliza anataka ndizi ngapi.





“Ngoja nifanye hesabu. Nadaiwa na Koba ndizi tatu, na Mzee Kigo ndizi nne. Kwa hiyo hasi tatu jumlisha hasi nne ni hasi saba. Kumbe nahitaji ndizi saba.”

$$(-3) + (-4) = -7$$




Ngedere alichanganyikiwa na maongezi ya hesabu, kwa hiyo alimuomba Kiduchu amueleweshe. “**Hasi** inamaanisha pungufu ya sifuri. Kama kudaiwa kitu.”



hasi

“Kama sidaiwi chochote je?
Kama ndizi zote ni zangu?”




hasi





“Hali kama hiyo tunaiita **CHANYA**.
Namba yeyote ambayo ni kubwa
kuliko sifuri ni **chanya**.”



Ngedere akampa Kiduchu ndizi. Kiduchu akaziangalia zile ndizi akaona zina jina la “Kigo” juu yake.




Hapo hapo akatambua zilikuwa ni zile zile ndizi alizozipata kutoka kwa Mzee Kigo ambazo zilipotea alipojikwaa.



Ngedere akaanza
kukimbia, lakini Kiduchu
akashika mkia wake.


“Njoo hapa wewe
mwizi wa ndizi!”
alilalama Kiduchu.




Ngedere aliomba msamaha na kumrudishia
Kiduchu ndizi alizomwibia.



Hakuishia hapo akampa ndizi tano zaidi ili
baadae Kiduchu amfundishe hisabati.



Kiduchu akaenda kwa Koba
na kumrudishia Koba ndizi tatu.





Baada ya hapo akaenda gengeni na kumrudishia Mzee Kigo ndizi zake. “Hii ni nini Kiduchu, hizi si zile zile ndizi nilizokupa?”



“Ni hadithi ndefu na inahusiana na mwizi wa ndizi. Nitakwambia siku nyingine. Kwa sasa chukua ndizi zako tatu. Na zawadi yako moja. Asante na kwaheri.”



“Ndizi moja...yote kwa ajili yangu!
Hatimaye nimepata namba chanya!”





Mwisho

Imeandaliwa na

ubongo.co

Haki zote zimehifadhiwa.
Hairuhusiwi kupiga chapa au kukitoa kitabu hiki kwa njia
ya aina yoyote bila idhini ya mwandishi,
UBONGO INTERNATIONAL.